

[Inicio](#) > [Adhana Kwa Mtazamo wa Qurani na Sunna](#) > Adhana: Sheria Na Vipengele Vyake Kwa Mujibu Wa Kitabu Na Sunna

---

## Adhana: Sheria Na Vipengele Vyake Kwa Mujibu Wa Kitabu Na Sunna

Kila sifa njema ni zake Mwenyezi Mungu mlezi wa ulimwengu.

Rehma na Amani zimfikie mbora wa viumbe na hitimisho la mitume wake, pia kizazi chake kitakatifu ambacho ndicho kasha la elimu yake na hazina ya mafunzo yake. Hakika Uislamu ni imani na sheria. Imani ni kuamini Mwenyezi Mungu, mitume wake na siku ya mwisho.

Na sheria ni hukumu za Mwenyezi Mungu ambazo zinajukumu la kumpa mwanadamu maisha bora na kumhakikishia wema wa dunia na Akhera.

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake, hivyo Mwenyezi Mungu akasema:

**الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ  
الْإِسْلَامَ دِينًا**

**“Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu.. ( 5:3 ).**

Isipokuwa kuna masuala madogo madogo ambayo wanazuoni wa sheria wameikhtilafiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu riwaya ambazo zimenasibishwa kwa Mtume. Jambo ambalo limepelekea kutofautiana kuhusu masuala madogo madogo ya sheria.

Kwa kuwa ukweli hutokana na utafiti, basi hakika katika mtiririko wa masomo haya tumejaribu kuliweka sala hili juu ya meza ya utafiti, kwani huenda ikawa ndio njia ya kuunganisha mtazamo na kusogeza hatua katika uwanja huu. Kwani tofauti iliyopo si katika asili na misingi ya dini hata ipelekee kuwa na uadui na chuki, bali tofauti iliyopo ni kuhusu riwaya zilizonasibishwa na Mtume, nalo ni jambo dogo ukilinganisha na mambo mengi ambayo tunaafikiana kati ya madhehebu za kiislamu. Na muongozo wetu katika njia hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

وَأَعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا ۗ وَادْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا

**Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, mlipokuwa maadui na akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema zake mkawa ndugu.” (3:103).**

**Ja’far Subhani**

**Tasisi ya Imam Sadiq ( a.s.)**

**Qum**

\*\*\*

Imam Ja’far Sadiq (a.s.) aliambiwa: ”Wanadai kuwa kuna mtu kati yaAnswari aliona adhana usingizini.” Imam akajibu: Wamesema uongo, hakika dini ya Mwenyezi Mungu ni takatifu zaidi ya kuonekana usingizini.”

Muhammad Al-Hanafiya amesema: ”Mmelizushia uongo jambo ambalo lina asili ndani ya sheria ya Uislamu na mafunzo ya dini yenu, hivyo mkadai eti lilitokana na ndoto aliyoiona mtu kati ya Answari usingizini mwake. Ndoto ambayo huenda ikawa ni uongo au kweli, na huenda ikawa si chochote.”

---

**URL del envío:** <http://www.al-islam.org/es/node/23245>